# MKATABA WA UWEKEZAJI KWA WACHIMBAJI WADOGO WENYE PML (PRIMARY MINING LICENSE)

Makubaliano haya yanafanywa na kukubaliwa leo hii tarehe..30.....mwezi...........01..........., 2024.

**KATI YA**

1. Abubakari Ibrahim Mwandulu
2. Ibrahim Mwandulu
3. Shabani Ibrahim Mwandulu
4. Maneno Rocky Malekela
5. Loveness Kavishe
6. Fatuma Ibrahim Mwandulu
7. Revocatus James Ngiyu

Waliotajwa hapo juu watajulikana kwa pamoja kama ("Wamiliki") wenye Leseni ya PML (Primary Mining License): **PML2404MOR & PML2403MOR**

**NA**

UHUSIANO INTERNATIONAL ICT LIMITED ni kampuni ya dhima ndogo iliyosajiliwa chini ya Sheria namba 12 ya mwaka 2002 ya Makampuni, ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya P.O Box 21189 Dar es Salaam inayojulikana kama ("Mwekezaji") ambapo muktadha unakubalika ni pamoja na warithi na kugawa kwa hatimiliki. sehemu nyingine.

## 1. MAKUBALIANO

Katika mkataba huu wamiliki wenye leseni tajwa hapo juu wanamiliki jumla ya hisa 200 zenye thamani ya kila hisa Tanzania shilling milioni mbili 2,000,000/= sawa na jumla ya Tanzania shilling millioni mia nne (400,000,000/=) ya his azote.
Katika mkataba huu wamiliki wamekubali katika jumla ya hisa 200 walizonazo kubakiwa na asilimia ishirini (20%) ya hisa sawa na hisa 40 yenye thamani ya milioni 80,000,000/= na mwekezaji kupata asilimia themanini (80%) ya hisa sawa na hisa 160 yenye thamani ya milioni 320,000,000/= kwa masharti yafuatayo:

1. kwa kuwa waliotajwa hapo juu ndio wenye haki na umiliki wa eneo , uchimbaji na umiliki wa madini katika leseni zilizotajwa hapo juu kwa mujibu wa sheria za madini ya mwaka 2017 na kanuni zake ya mwaka 2018 , mwekezaji atalazimika kununua hisa asilimia themanini (80%) za umiliki wa madini na uchimbaji kutoka kwa wamiliki waliotajwa katika leseni tajwa hapo juu.
   Kila hisa moja inayomilikiwa inathamani ya Tanzania shilingi milioni mbili (Tsh 2,000,000/=) kwaiyo mwekezaji atalazimika kuwalipa wamiliki jumla ya Tanzania shilling



Scanned with CamScanner

milioni mia tatu na ishirini tu (TZS 320,000,000) sawa na hisa mia moja na sitini (160) sawa na asilimia 80% ya hisa zote kutoka wamiliki wa mgodi.
Kwa mujibu wa makubaliano maalumu za pande zote mbili wamiliki wamekubali mwekezaji atalipa jumla ya Tanzania shilingi milioni mia mbili na hamsini (250,000,000/=) badala ya Tanzania shilling milioni mia tatu na ishirini (TZS 320,000,000) kwa hisa 160 sawa asilimia 80% ya hisa zote kwa wamiliki wa leseni tajwa hapo juu na wamiliki watabaki na hisa 40 sawa na asilimia 20% ya hisa zote .

2. Mgao wa dhahabu pia utafata asilimia hiyo ya 80% kwa 20% baada ya kutoa gharama zote za uendeshaji, kwa mfano kama kilo moja ya dhahabu ina thamani ya millioni mia na hamsini (TZS 150,000,000) na gharama za uendehsaji ni millioni mia moja (TZS 100,000,000) faida itabaki millioni hamsini (TZS 50,000,000) ambayo asilimia 80% sawa sawa na million arobaini (TZS 40,000,000) itakwenda kwa mwekezaji na asimilia ishirini 20% sawa sawa na millioni kumi (TZS 10,000,000) itakwenda wa wamiliki wa mgodi.

3. Pesa hiyo italipwa kwenye akaunti ya muhasibu wa wamiliki wa mgodi ambaye ni SHABANI IBRAHIM MWANDULU mwenye akaunti namba 0152319252500 jina la bank CRDB na jina la akaunti SHABANI IBRAHIM MWANDULU, na wamiliki wanaweza wakabadilisha akaunti na kumtaarifu mwekezaji.

4. Dhahabu itakayotokana na marudio au seneti hayatatolewa gharama za uendeshaji na itafata mgao wa asilimia 80% kwa 20% kwa mujibu wa makubaliano haya.

5. Gharama za kodi na tozo zitakazotokana na dhahabu iliyozalishwa katika mgodi au kutoka kwenye marudio/seneti (royalty fees) zitafanywa na mwekezaji katika ile asilimia themanini (80%) na gharama za kodi na tozo zitakazotokana na dhahabu iliyozalishwa katika mgodi au kutoka kwenye marudio/seneti (royalty fees) zitafanywa na wamiliki katika ile asilimia ishirini (20%) yao.

6. Uhusiano mining group limited itafanya shughuli zote za uendeshaji na usimamizi wa mgodi.

7. Mwekezaji atalazimika kwa mujibu wa sheria za madini na kanuni zake kutoa huduma kwa Jamii na kwa wamiliki wa mgodi pale huduma itakapohitajika baada ya kupelekewa maombi.

## 2. USIMAMIZI

Usimamizi wote na shughuli zote za uendehsaji katika mgodi utakuwa chini ya mwekezaji, isipokua wamiliki watalazimika kuingizwa katika usimamizi kwa kusimamia hisa zao kwa mujibu wa sheria za hisa katika makampuni:



Scanned with CamScanner

1. Wamiliki wataruhusiwa kutembelea eneo la mgodi ili kujua maendeleo ya mgodi.
2. Wamiliki wataruhusiwa kukagua wakati wa uzalishaji wa dhahabu unafanyika.
3. Wamiliki wanahaki kupata taarifa za mahesabu.
4. Wamiliki wanahaki ya kuhudhuria vikao vya wakurugenzi wa kampuni vinavyohusu uendeshaji wa mgodi kwa mujibu wa sheria za hisa na mwekezaji atatoa taarifa kwa wamiliki kwa nia nzuri (good faith).

## 3. MWISHO WA MKATABA

Kutokana na sheria ya madini ya mwaka 2017 juu ya haki ya umiliki wa madini ambao kibali chake ni leseni zinazotolewa kwa mujibu wa sheria hiyo. Kwa maana hiyo uhai wa mkataba huu utafatana na uhai au ukomo wa leseni ambao ni miaka saba yaani tarehe 01/12/2030, kama mmiliki atarenew leseni mkataba huu utaingiwa tena.

Kwa mkataba huu wamiliki wa leseni na mgodi tajwa hapo juu kwa upande mmoja na kampuni ya wawekezaji kwa upande wa pili hawataingia mkataba mwingine wowote nje ya mkataba huu kwa eneo la mgodi wenye leseni tajwa hapo juu.

## 4. UTATUZI WA MIGOGORO

1. Mzozo au kutokuelewana yoyote ambayo inaweza kutokea au ambayo ni kushikamana au tukio la utekelezaji wa Mkataba huu itatatuliwa kwa amani katika mikutano ya kawaida inayoitishwa na upande ulioadhilika ndani ya siku 90. Iwapo hakuna suluhu inayoweza kufikiwa ndani ya siku 180 baada ya mmoja wa upande mmoja kupokea taarifa ya maandishi ya mgogoro kutoka kwa upande mwingine, utata wowote kama huo, madai au mgogoro unaohusiana na au unaotokana na Mkataba huu utasuluhishwa na kwa upekee. kwa mujibu wa Sheria ya Usuluhishi ya Tanzania.

2. Mahali pa usuluhishi patakuwa Dar es Salaam au Morogoro,

3. Chama cha Morogoro Earth Miners Association watahusishwa wakati wowote utakapotokea mgogoro

Mkataba huu na makubaliano haya yatatambulika kwa mujibu wa sheria ya mikataba ya Tanzania na sheria ya madini na iwapo kutakuwa na kutokubaliana, mgogoro huo utatuliwe kama inavoelezea katika aya ya 4 ya makataba huu.

## 5. KUVUNJWA KWA MKATABA.

Pande zote zina haki ya kuvunja mkataba iwapo pande moja itakiuka na kwenda kinyume na kifungu cha kwanza na cha pili cha mkataba huu baada ya kutoa notisi ya siku 90.



Scanned with CamScanner

Makubaliano haya ya uwekezaji yanashuhudiwa na kusainiwa hapa Morogoro na hawa wafuatao.

**WAMILIKI**

| Jina | Saini |
|---|---|
| 1. Maneno Rocky Malekela | ………………………… |
| 2. Ibrahim Mwandulu | ………………………… |
| 3. Shabani Ibrahim Mwandulu | ………………………… |
| 4. Abubakari Ibrahim Mwandulu | ………………………… |
| 5. Loveness Kavishe | ………………………… |
| 6. Fatuma Ibrahim Mwandulu | ………………………… |
| 7. Revocatus James Ngiyu | ………………………… |

**MASHAHIDI KWA UPANDE WA WAMILIKI**

1. Jina ……………………………………… CEO Morogoro Earth Miners Association

   Saini ………………………

2. Jina ……………………………… Saini ……………………

**MWEKEZAJI (UHUSIANO INTERNATIONAL ICT LIMITED)**

Mkurugenzi mkuu

Jina Samir Huzaifa Mulla……………………………… Saini ……………………

UHUSIANO INTERNATIONAL ICT LTD.
P.O. Box 34674
DAR-ES-SALAAM



Scanned with CamScanner

**MASHAHIDI WA MWEKEZAJI**

1. Jina HASSAN RAMADHANI MHETO.................... Mkurugenzi Mkuu UHUSIANO MINING GROUP LIMITED Saini.................................

2. Jina Asifiwe Alinanuswe.................... Saini.................................

Scanned with CamScanner

**MUHTASARI WA KIKAO CHA WAMILIKI WA LESENI ZA UCHIMBAJI MDOGO WA MADINI NAMBA PML2403MOR NA PML2404MOR KILICHOFANYIKA TAREHE 26 JANUARI 2024 KATIKA OFISI YA WAMILIKI ILIYOPO SOKO LA KINGALU MOROGORO MJINI (MANISPAA)**

**WALIOHUDHURIA KIKAO**

1. MANENO ROCK MALEKELA - MWENYEKITI
2. ABUBAKARI IBRAHIMU MWANDULU - KATIBU
3. IBRAHIMU B. MWANDULU
4. SHABANI IBRAHIMU MWANDULU
5. FATUMA IBRAHIMU MWANDULU

**WASIOHUDHURIA KWA TAARIFA**

1. LOVENESS KAVISHE
2. REVOCATUS JAMES NGIYU

Kikao kimefunguliwa na mwenyekiti majira ya saa 11 jioni, mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa kuhudhuria kikao cha dharula ambacho agenda zake zitasomwa na katibu, mwenyekiti aliwataka wajumbe kuwa makini na kujadili agenda yao kwa uhuru kwani inagusa maslahi ya wamiliki wenyewe.

**AGENDA ZA KIKAO**

**1. YAHUSU UWEKEZAJI KATIKA MGODI WENYE LESENI NAMBA PML 2403MOR NA PML 2404MOR ILIYOPO MELELA**

**2. YAHUSU MALIPO YA UHAMISHO WA HISA 160 KUTOKA KWA WAMILIKI WA LESENI NAMBA PML 2403MOR NA PML 2404MOR KWENDA KWA WAWEKEZAJI**

**3. YAHUSU RIDHAA YA UHAMISHO WA HISA**

**YAHUSU UWEKEZAJI KATIKA MGODI WENYE LESENI NAMBA PML 2403MOR NA PML 2404MOR ILIYOPO MELELA**

Katibu aliwaeleza wajumbe wa kikao kuwa kampuni ya UHUSIANO INTERNATIONAL ICT LIMITED imefanya mabadiliko ya kimuundo na kiutendaji kutoka kuwa WAWEZESHAJI hadi

Scanned with CamScanner

kuwa WAWEKEZAJI katika mgodi wenye leseni namba PML2403MOR na PML2404MOR.Kwa hiyo wajumbe mnatakiwa kujadili kwa kina kuhusu mchakato wa kubadilika kwa mfumo kwenda kwenye UWEKEZAJI.

Baada ya mjadala mzito wajumbe kwa pamoja wameridhia kwa kauli moja kukubali kampuni ya UHUSIANO INTERNATIONAL ICT LIMITED kuwa WAWEKEZAJI kama walivyoomba.

**YAHUSU MALIPO YA UHAMISHO WA HISA 160 KUTOKA KWA WAMILIKI WA LESENI NAMBA PML 2403MOR NA PML 2404MOR KWENDA KWA WAWEKEZAJI**

Katibu aliwaeleza wajumbe kuwa kampuni ya UHUSIANO INTERNATIONAL ICT LIMITED imewaomba wamiliki kuwahamishia hisa walizonazo kwa asilimia themanini (80%) sawa na hisa mia moja na sitini (160) zenye thamani ya shilingi milioni mia tatu na ishirini (320), pia waliwaomba wamiliki wao watawalipa kiasi cha shilingi milioni mia mbili na hamsini (250) badala ya shilingi milioni mia tatu na ishirini (320) sawa na hisa mia moja na sitini (160).

Wajumbe walilijadili swala hili la malipo kwa mvutano mkubwa kutokana na kwamba hawakuona sababu ya malipo hayo kupunguzwa ikizingatiwa kuwa mgodi baada ya utafiti kufanyika na kuthibitisha kuwa na deposit ya dhahabu kilo mia sita (600), kwa makadilio ya shilingi bilioni mia moja na moja (bilioni 101) kwa kuzingatia kuwa kiasi cha shilingi milioni mia tatu na ishirini ni kiasi kidogo kwa malipo ya wamiliki wenyewe, hata hivyo baada ya mjadala mzito wenye mvutano ulioishia kwa wajumbe kupiga kura.

Wajumbe waliohafiki malipo hayo ya shilingi milioni mia mbili na hamsini (250) walishinda kwa kura 3 dhidi ya kura 2 ambao hawakuhafiki malipo ya shilingi milioni mia mbili na hamsini (250).

Hivyo kikao kilikubaliana wamiliki kulipwa shilingi milioni mia mbili na hamsini (250) bila masharti yeyote na zilipwe fedha taslimu.

**YAHUSU RIDHAA YA UHAMISHO WA HISA**

Katibu aliwaeleza wajumbe kwa mujibu wa sheria wamiliki wanalazimika kuhamisha hisa zao walizokubaliana hisa mia moja na sitini (160) zenye thamani ya shilingi milioni mia tatu na ishirini (320) ambazo kwa makubaliano maalumu wameridhia kulipwa shilingi milioni mia mbili na hamsini (250).

Hivyo aliwaeleza wajumbe kuwa uhamisho huo utafanyika baada ya malipo yote kufanyika pasipo kusahau malipo ya CAPITAL GAIN TAX(CGT) yatalipwa na wawekezaji ambao ni kampuni ya UHUSIANO INTERNATIONAL ICT LIMITED kwa mujibu wa sheria. Wajumbe walijadili swala ilo kwa maelewano makubwa kutokana na agenda yenyewe kujitosheleza.

Scanned with CamScanner

**MAAZIMIO YA KIKAO**

Kutokana na mijadala ya agenda zote tatu zilizojadiliwa katika kikao hiki, kikao kinatoa tamko rasmi kama maamuzi ya wamiliki wa mgodi wenye leseni namba PML 2403MOR na PML 2404MOR leo tarehe 26 mwezi Januari mwaka 2024 kwamba :-

Wamiliki kwa pamoja katika kikao chao halali wameamua bila shindikizo lolote kuzitoa hisa mia moja na sitini (160) sawa na asilimia themanini (80%) kwa mwekezaji ambayo ni kampuni ya UHUSIANO INTERNATIONAL ICT LIMITED, kwa hiyo kwa asilimia (80%) ya hisa 200 sawa na hisa mia moja na sitini (160) zenye thamani ya shilingi milioni mia tatu na ishirini (320) ambazo kwa makubaliano ya pande zote mbili kwa mwekezaji kulipa shilingi milioni mia mbili na hamsini (250M).

Kwa hisa hizo za asilimia themanini (80%) sasa kampuni ya UHUSIANO INTERNATIONAL ICT LIMITED ndio itakayokuwa mwendeshaji mkubwa wa mgodi hivyo kuipa haki ya kuchimba na kumiliki madini ya dhahabu tu na iwapo kutapatikana madini mengine yatakuwa chini ya wamiliki wa mgodi.

**MENGINEYO**

Kwa ruhusa ya mwenyekiti, mjumbe mmoja aliwakumbusha wamiliki kwa kuwaeleza kuwa kinachofanyika ni kuhamisha hisa na sio kuuza mgodi kwa hiyo haki ya umiliki wa mgodi kwa maana ya leseni namba PML 2403MOR na PML 2404MOR zitabaki kwa wamiliki wenyewe kwa hiyo kampuni ya UHUSIANO INTERNATIONAL ICT LIMITED itabaki na haki ya kumiliki madini (MINERAL RIGHTS) sawa na wamiliki wa mgodi.

Mjumbe mwingine aliwatahadhalisha wajumbe kuwa wao ndio wenye haki ya umiliki wa ulinzi wa mgodi kwa mujibu wa sheria hivyo kuwataka kuwa makini na kusiwe na hujuma ya utoroshaji wa madini na kuwataka kampuni ya UHUSIANO INTERNATIONAL ICT LIMITED kufanya kazi kwa uadilifu na uwazi.

**KUFUNGA KIKAO**

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe na michango yao ya mijadala pamoja na changamoto ya mivutano ya hapa na pale yenye tija ya kujenga na kulinda maslahi na kuamua kufunga kikao mnamo saa 1:00 usiku.

Muhtasari huu umethibitishwa,

| | |
|---|---|
| ................................ | ................................ |
| ABUBAKARI IBRAHIMU MWANDULU | MANENO ROCK MALEKELA |
| KATIBU | MWENYEKITI |

Leo tarehe 30.01.2024

Scanned with CamScanner

# HATI YA UHAMISHO WA HISA

Hati hii ya **UHAMISHO WA HISA** unafanywa kati ya wamiliki wa mgodi wenye leseni namba **PML2403MOR na PML2404MOR** kwa mujibu wa hati hii wanajulikana kama **WAHAMISHAJI WA HISA (TRANSFEROR/SELLER)**

**Na**

Kampuni ya **UHUSIANO INTERNATIONAL ICT LIMITED** hapa wanajulikana kama **WAHAMISHIWAJI WA HISA (TRANSFEREE/PURCHASER)**

Wamiliki wa mgodi wamekubali kuhamisha jumla ya hisa zao mia moja na sitini (160) kwa mujibu wa kikao cha dharula kilichofanyika mnamo tarehe 26/01/2024 na kutolewa maamuzi haya.

Kampuni ya **UHUSIANO INTERNATIONAL ICT LIMITED** wamekubali kupokea uhamisho wa hisa mia moja na sitini (160) kutoka kwa wamiliki wa mgodi wenye leseni namba **PML2403MOR na PML2404MOR**.

Hati hii imesainiwa leo tarehe …30…. Mwezi …01……… mwaka 2024…… kati ya :-

**WAHAMISHAJI (Wamiliki wa leseni namba PML2403MOR na PML2404MOR)**

1. MANENO ROCKY MALEKELA ……………………………
2. ABUBAKARI IBRAHIMU MWANDULU …………………………..
3. IBRAHIMU B. MWANDULU ………………………………
4. SHABANI IBRAHIMU MWANDULU ……………………
5. FATUMA IBRAHIMU MWANDULU ………………………
6. LOVENESS KAVISHE ……………………
7. REVOCATUS JAMES NGIYU ………………………..

**Na**

**WAHAMISHIWAJI (Wawekezaji Kampuni ya UHUSIANO INTERNATIONAL ICT LIMITED)**

………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………

Scanned with CamScanner


PML2403MOR


ANNEX A

## DESCRIPTION OF THE PRIMARY MINING LICENCE AREA

The Primary Mining Licence is at **Melela Mlandizi** area in **Mvomero** District, QDS **182/4** defined by the following corner co-ordinates (Arc 1960):

| Corner | Latitude | Longitude |
|---|---|---|
| 1 | - 06 deg. 58 min. 10.00 sec. | 37 deg. 25 min. 11.00 sec. |
| 2 | - 06 deg. 58 min. 17.00 sec. | 37 deg. 25 min. 11.00 sec. |
| 3 | - 06 deg. 58 min. 17.00 sec. | 37 deg. 25 min. 3.00 sec. |
| 4 | - 06 deg. 58 min. 10.00 sec. | 37 deg. 25 min. 3.00 sec. |




| Legend | |
|---|---|
| Licensed area |  |
| License Number | PML2403MOR |
| District | Mvomero |
| Direction | N |

An area of approximately **5.28** Hectares.

## ANNUAL RENT PAYMENTS

| Year | ERV | Amount (TShs.) | Date | Signature & Stamp |
|---|---|---|---|---|
| 1. | 923330216865723 | 475,200/= | 26.11.2023 | RESIDENT MINES OFFICER MOROGORO |
| 2. | | | | |
| 3. | | | | |
| 4. | | | | |
| 5. | | | | |
| 6. | | | | |
| 7. | | | | |




Scanned with CamScanner

## ANNEX A

### DESCRIPTION OF THE PRIMARY MINING LICENCE AREA

The Primary Mining Licence is at **Mlandizi** area in **Mvomero** District, QDS **182/4** defined by the following corner co-ordinates (Arc 1960):

| Corner | Latitude | Longitude |
|---|---|---|
| 1 | - 06 deg. 58 min. 17.00 sec. | 37 deg. 25 min. 11.00 sec. |
| 2 | - 06 deg. 58 min. 17.00 sec. | 37 deg. 25 min. 17.00 sec. |
| 3 | - 06 deg. 58 min. 10.00 sec. | 37 deg. 25 min. 17.00 sec. |
| 4 | - 06 deg. 58 min. 10.00 sec. | 37 deg. 25 min. 11.00 sec. |




| Legend | |
|---|---|
| Licensed area | 1 2 4 3 |
| License Number | **PML2404MOR** |
| District | **Mvomero** |
| Direction | N |

An area of approximately **3.96** Hectares.

### ANNUAL RENT PAYMENTS

| Year | ERV | Amount (TShs.) | Date | Signature & Stamp |
|---|---|---|---|---|
| 1. | 923330216865566 | 356,400/= | 26.11.2023 | MOROGORO |
| 2. | | | | |
| 3. | | | | |
| 4. | | | | |
| 5. | | | | |
| 6. | | | | |
| 7. | | | | |

Scanned with CamScanner

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
**MINISTRY OF MINERALS**

**MINING COMMISSION**

THE MINING (MINERAL RIGHTS) REGULATIONS, 2018
**PRIMARY MINING LICENCE PML2403MOR**
***The Mining Act, Cap. 123***

The exclusive right, subject to the provisions of ***The Mining Act, Cap. 123*** and the regulations made thereunder or which may come into force during the continuance of this primary mining licence or any renewal thereof is hereby granted to M/S **Ibrahim Bakari Mwandulu** of **P. O. Box 34267, Dar es Salaam – Tanzania,** in partnership with **Fatuma Ibrahim Mwandulu, Revocatus James Ngiyu and Shabani Ibrahim Mwandulu** (hereinafter called the Licensee), to prospect and mine for **Gold**, at **Melela Mlandizi** in **Mvomero** District, QDS **182/4** over an area described overleaf (Annex A).

This Licence, unless sooner cancelled, suspended or surrendered pursuant to the provisions of ***The Mining Act, Cap. 123*** shall be valid for a period of **seven (7)** years, effective from the date of grant.

Granted this ....01.... day of ....DECEMBER.... 2023

...........................................................
Eng. Lucas D. Mlekwa
For: **EXECUTIVE SECRETARY**

Scanned with CamScanner

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
**MINISTRY OF MINERALS**

**MINING COMMISSION**

THE MINING (MINERAL RIGHTS) REGULATIONS, 2018
**PRIMARY MINING LICENCE PML2404MOR**
***The Mining Act, Cap. 123***

The exclusive right, subject to the provisions of ***The Mining Act, Cap. 123*** and the regulations made thereunder or which may come into force during the continuance of this primary mining licence or any renewal thereof is hereby granted to M/S **Ibrahim Bakari Mwandulu** of **P.O. Box 34267 Dar es Salaam – Tanzania, ,** in partnership with **Abubakar I Mwandulu, Loveness Kawiche, Maneno Rocky Malekela, Shabani Ibrahim Mwandulu** (hereinafter called the Licensee), to prospect and mine for **Gold**, at **Mlandizi,** in **Mvomero** District, QDS **182/4** over an area described overleaf (Annex A).

This Licence, unless sooner cancelled, suspended or surrendered pursuant to the provisions of ***The Mining Act, Cap. 123*** shall be valid for a period of **seven (7)** years, effective from the date of grant.

Granted this ......01...... day of ......DECEMBER...... 2023

.............................................................

Eng. Lucas D. Mlekwa
For: **EXECUTIVE SECRETARY**



Scanned with CamScanner